

# MKATABA WA UNUNUZI WA Eneo

Kati ya

**BENITHO MWALONGO** (ambaye hapa atajulikana muuzaji kwa upande mmoja )

Na

**AM JOLDAN LIMITED** (amabaye atajulikana Mnunuzi kwa upande mwingine )

*Makataba wa mauziano umefanyika mnamo leo tarehe .....<sup>02</sup>..... Mwezi .....<sup>02</sup>... Mwaka <sup>2023</sup>*

**MAKUBALIANO**

Makubaliano haya yamefanyika leo .....02.....mwezi wa.....02.....2023

Kati

**BENITHO MWALONGO** wa S.L.p.....Makambako, Njombe (ambaye katika Mkataba huu ataitwa "MUUZAJI") kwa upande mmoja.

Na

**AM JOLDAN LIMITED** ya S.L.P 79, Makambako - Njombe, kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni ya mwaka 2002 na kupewa cheti namba 133957 (ambayo katika Mkataba huu itajulikana kama "MNUNUZI") wa upande mmoja

**AMBAPO MUUZAJI** ni mmiliki halali wa eneo lisilopimwa lililopo CHALOWE, ..... katika Wilaya ya CHALOWE Mkoa wa Njombe lenye ukubwa wa upana hatua .....(.....) na urefu wa hatua .....(.....) na pia mipaka yake ni kama ifuatavyo:-

1. Mashariki linapakana na KADUMA
2. Magharibi linapakana na KADUMA
3. Kaskazini linapakana na KADUMA
4. Kusini linapakana na BARABARA

NA **AMBAPO MUUZAJI** ana nia ya kuuza eneo lake kwa **MNUNUZI** kwa thamani ya fedha za Kitanzania Shilingi Million .....ONE TU..... (Tshs. 4,000,000...../=) tu na **MNUNUZI** ana nia thabiti ya kununua eneo hilo kwa thamani ya fedha za Kitanzania Shilingi .....ONE TU..... (Tshs. 4,000,000...../=) tu.

NA **AMBAPO PIA MNUNUZI** anatamani kupokea malipo tajwa hapo juu kwa awamu kadhaa kupitia malipo kidogo kidogo kama ambavyo yataonyeshwa kwenye jedwali mwishoni mwa mkataba huu.

**SASA BASI MKATABA HUU UNASHUHUDIWA KAMA IFUATAVYO: -**

- (a) **MUUZAJI** ameua na **MNUNUZI** amenunua eneo hilo kwa makubaliano yaliyowekwa na si vinginevyo.
- (b) **MUUZAJI** anamhakikishia **MNUNUZI** kuwa ni mmiliki halali wa eneo hilo liliopo kijiji cha **CHALOWE** na ana mamlaka ya kuuza kama anavyofanya sasa, na familia yake na warithi pia wameridhia kuhusiana na mauziano haya.
- (c) **MUUZAJI** ameua eneo hilo kwa kiasi cha Shilingi za Kitanzania Milioni .....ONE TU (Tshs. 4,000,000...../=) tu na ambapo utaratibu wa malipo utaonyeshwa kwenye jedwali mwisho mwa mkataba huu.
- (d) **MUUZAJI** atamkabidhi rasmi **MNUNUZI** eneo husika liwe mali yake halali pamoja na nyaraka zote zinazohusiana na umiliki wa eneo hilo na alitumie kadri awezavyo kulingana na sheria za nchi mara baada ya kuanza kulipa awamu ya kwanza ya malipo.
- (e) **MUUZAJI** anamhakikishia **MNUNUZI** kuwa atashirikiana naye katika suala zima la uhamishaji wa umiliki wa eneo hilo katika vyombo husika.

- (f) MUUZAJI anamhakikishia MNUNUZI kuwa eneo hilo halina madai yoyote na anaahidi kumlinda na kushughulikia kwa gharama zake mwenyewe endapo madai yoyote yatajitokeza dhidi ya eneo husika.
- (g) MUUZAJI anakubaliana na MNUNUZI kwamba endapo utajitokeza mgogoro wowote utakaosababisha MNUNUZI kunyang'anywa umiliki wa eneo husika basi MUUZAJI atamfidia MNUNUZI kama ifuatavyo.
- i. MUUZAJI atamrejeshea MNUNUZI fedha zote za mauzo ya eneo zitakazokuwa zimelipwa kwa mujibu wa Mkataba huu;
  - ii. MUUZAJI atamlipa MNUNUZI riba ya asilimia ishirini na tano (25%) kwa kila siku ya thamani ya mauzo ya eneo kwa mujibu wa Mkataba huu ambayo itatozwa kwa kila siku moja kuanzia tarehe ya kusaini Mkataba huu hadi mgogoro husika utakapokwisha;
  - iii. MUUZAJI atamlipa MNUNUZI fidia ya maendeleo yote ambayo MNUNUZI atakuwa ameyafanya katika eneo husika.
- (h) Kwamba, upande wowote utakaokiuka mkataba huu, upande ulioathirika una haki ya kwenda mahakamani kwa mujibu wa sheria za Nchi.
- (i) Kwamba makubaliano haya ni ya kudumu na yatazibana pande zote mbili, warithi na wawakilishi wao.

KWA KUSHUHUDIA pande zote mbili zikiwa na akili timamu na bila kulazimishwa na baada ya kusomewa, kuelewa na kuridhia masharti yote yalipo katika mkataba huu, zimeweka saini zao hapa Makambako katika tarehe, mwezi na mwaka kama inavyoonyesha hapa chini:-

UMESAINIWA na KUWAKILISHWA hapa  
 MAKAMBAKO na BENITO MUDSONTO  
 ambaye namfahamu binafsi/ametambulishwa  
 kwangu na ..... ambaye  
 namfahamu binafsi mbele yangu leo tarehe  
 tarehe 02 mwezi 02 2023

MUUZAJI

MBELE YANGU:

Jina GLADNESS FUNGO

Saini: [Signature]  
 Wadhifa: Wakil wa Kujitegemea



MASHAHIDI WA MUUZAJI:

1. Jina: ADAM NAKALI NGAMPUDZI

Saini: [Signature]  
 Uhusiano: KAKA


2. Jina: .....

Saini: .....

Uhusiano: .....

**MBELE YANGU:**

Jina: GLADNESS FUNGO

Saini:  .....

Wadhifa: Wakili wa Kujitegemea



UMEWEKWA LAKIRI ya kampuni ya AM  
JOLDAN Limited hapa MAKAMBAKO leo  
tarehe 02 mwezi 02 mwaka 2023

**SHUHUDA WA KAMPUNI:**

Jina: ANSON M. MKANE

Saini: AMAKAMBAKO

Cheo: Mkurugenzi wa Kampuni

**MBELE YANGU:**

Jina: GLADNESS FUNGO

Saini:  .....

Wadhifa: Wakili wa Kujitegemea

